

**ALLIANCE HIGH SCHOOL
KISWAHILI KIDATO CHA 3
MUHULA WA I,
MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA 2016**

MAAGIZO

1. *Karatasi hii ina maswali matano*
2. *Maswali yote ni ya (azima)*
3. *Jibu maswali katika nafazi ulizoachiwa baada ya kila swali.*
4. *Karatasi hii ina alama 100.*

1. Ufahamu (alama 15)

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali

Takwimu za tafiti za umaskini kila mara huonyesha kuwa bara la Afrika ndilo bara maskini kabisa kote duniani. Takriban wakaazi kiasi cha asilimia themanini hawawezi kumudu kutumia dola moja kwa siku. Toka Kaskazini hadi Kusini, Mashariki hadi Magharibi mwa bara, makaazi ya vibanda yametamalaki. Wakaazi wengi hulala njaa kutokan na ukosefu wa chakula.

Watu wa mitaani waliovaa mararururu wamejaa katika miji ya bara hili. Swali ni; Je, Kwa nini umaskini umeliganda bara la Afrika hivi mithili ya kupe? Kwa nini bara huselea katika lindi la uchochole?

Ili kuelewa sababu za umaskini kuganda barani Afrika, yampasa mtu ima fa ima kurejelea historia ya bara hili. Kwa kipindi cha karne nyingi, Afrika ilidhibitiwa na walowezi pamoja na mabeberu. Wana wake ambao wangelistawisha bara hili kiuchumi walitwaliwa kimabavu na kupelekwa, huku wamefungwa minyororo, kustawisha uchumi wa maara mengine. Afrika ikaporwa nguvu ambayo ni rasilimali kuu katika ustawishaji wa uchumi. La kusikitisha ni kuwa Afrika haikufidiwa kutokana na wizi huu. Badala yake iliongezewa mizigo mingine.

Baada ya kipindi cha biashara ya utumwa kumalizika, Afrika ilijipata katika janga jingine. Wakoloni wakaliingilia bara kwa pupa. Wakaligawanya katika koloni mbalimbali miononi mwao. Wakaingiwa na wendawazimu kuiba malighafi ya bara hili. Wakaiba mashamba, madini, miti na chochote cha maana walichokipata. Badala ya malighafi haya kutumika kunawirisha bara la Afrika, yalitwaliwa kustwisha chumi za walikotoka wakoloni. Afrika ikaachwa kuzidi kudidimia katika lindi la umaskini.

Wakoloni walipotoka barani Afrika na kuzipa dola nyingi za Afrika "Uhuru", waliacha mkururo wa madhila. Madhila haya hayangeikubalia Afrika kujikomboa kutoka katika biwi la uchochole. Tatizo la kwanza na kubwa zaidi ni wakoloni kugawanya na kukatakata Afrika katika mataifa mengi. Mgawanyo huu ukawa haukufuata utaratibu wowote. Kwa sababu hii, watu wa nasaba moja wakawekwa katika nchi tofauti. Mathalani, watu wa nasaba ya Kisomali waligawanywa na kuwekwa chini ya nchi huru ya Somali, wengine wakawa nchini ya dola la Uhabeshi, huku wengine wakiwa nchini Kenya na Jibuti. Watu kama hawa hawakutaka mpango huu. Waliokuwa Kenya na Uhabeshi wakachukua silaha na kupigana ili warejeshwe chini ya himaya moja ya taifa huru la Somalia. Watu kama hawa wakatamia muda mwingi kupigana;

muda ambao ungetumika kuinua Afrika kiuchumi. Mpigano haya ya wenyewe kwa wenyewe yamekithiri kote katika bara la Afrika.

Halikadhalika, mkoloni hakufanya juhudi zozote za kuanzisha viwanda ambavyo vingenyanyua uchumi wa Afrika na kuwatoa waafrika katika biwi la ufukara. Palipokuwa na ari yoyote ya kuanzisha kiwanda, kilipoanzishwa hakikusaidia Afrika kiuchumi. Vilikuwa viwanda vya kupunguza zigo la bidhaa na kuzifanya kuwa nyepesi ili zisafirishwe kwa ajili ya viwanda vya nchi walizotoka wakoloni.

Kwa kipindi cha muda ambao mkoloni amekuwa na maingiliano na wakaazi wa Afrika, amehakikisha kuwa mwafrika amekuwa mtegemezi wake. Malighalifi ya Afrika yalipelikwa kutayarishiwa viwanda vya wakoloni. Kisha mwafrika alirudishiwa zikiwa bidhaa kamili za kutumiwa. Mwafrika akaonyeshwa kuwa chochote kilichotoka kwa wakoloni ni bora zaidi ya chake alichozalisha. Hii ikiwa ni mbinu moja ya wakoloni kuwafukarisha waafrika. Hata sasa, kilichotoka Ulaya, hata kama ni cha hali ya chini, huonekana bora zaidi kuliko alichozalisha mwafrika.

Kwa upande mwingine, inadhihirika kuwa wakoloni hawajawahi kuondoka na kuwaachia Waafrika jukumu kamili la kuendesha uhuru wao kisiasa, kijamii na kiuchumi. Waliondoka kupitia mlango mmoja na kurudi kwa wa pili. Mlango wa pili ukawa ni ukoloni kuchukua sura nyingine, sura ya ukoloni mamboleo. Kupitia ukoloni huu, wakoloni hudhibiti uchumi na maendeleo ya Afrika kupitia asasi mbili walizozianzisha, yaani Benki Kuu ya Dunia na shirika la Fedha Duniani. Ili kupata mikopo ya maendeleo, asasi hizi hutoa masharti ambayo hukwamiza badala ya kuchangia kuleta maendeleo barani Afrika.

Sasa hivi pana haja ya wana wa Afrika kufanya vikao vya dharura ili kujadiliana kuhusu suluhisho la tatizo hili sugu la umaskini barani. Lazima wawahimimize waafrika wote kujikomboa kiakili na kung'amua kuwa maendeleo ya bara lazima yaongozwe na yadhibitiwe na Waafrika wenyewe. Wawahimimize kuacha hulka za kukimbilia mataifa yaliyowafanya watumwa na kuwakalia kikoloni kwa misaada ya maendeleo. Misaada hii si ya dhati bali ni ya chati na hailengi kuondoa umaskini barani bali kuuendeleza.

Pana haja pia, Waafrika kuwa na miungano ya kiuchumi. Miungano hii husaidia katika uteteaji wa soko pamoja na bei za bidhaa zao ikilinganishwa na taifa moja kuyaendeleza mambo haya. Halikadhalika, waafrika wanapswa kutambua kile wanachotaka na kupanga mikakati ya kufikia mahitaji ya kimsingi kwa wananchi wake kwa mfano, uimarishaji wa mbinu msingi ambazo zitachangia kuimarisha uchumi wa mataifa wahitaji kuwa mstari wa mbele badala ya ununuzi wa magari na ndege za hadhi za kuwabebea viongozi.

Maswali.

a) Ipe taarifa hii mada mwafaka.

(Alama. 1)

b) Ni mambo gani yanadhihirisha kuwa umaskini umetamalaki, barani Afrika (alama 2)

c) Eleza sababu zinazochangia kuendeleza umaskni barani Afrika. (Alama 5)

d) Taja njia zinazoweza kukabiliana na umaskini barani Afrika. (alama 3)

e) Andika maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika taarifa (alama 4)

- i) Kuselea _____
- ii) Ima faima _____
- iii) Mkururo wa madhila _____
- iv) Malighafi _____

2. ufupisho alama 15

Soma habari ifatayo kisha ujibu

Zamani wanadamu wa maswali kwanza ambao ni mababu wa vizazi vingi vilivyopita waliishi duniani. Habari kuhusu maisha na maumbile yao haikujulikana kwa hakika kwa sababu hawakuwa na uwezo wa kuandika. Lakini mara kwa mara shughuli za wanaakioljia kama Louis Leakey na wengine hugundua mifupa ya ardhini na michoro yao katika mapango. Wataalamu hawa hufukua mafuvu, vyombo na silaha zao za zamani. Kwa kuchunguza vitu hivi tunaweza kubahatisha viumbe hawa walivyokuwa na jinsi walivyoishi.

Moja ya mambo yanayofahamika sasa ni kuwa wanadamu hawa wa awali walifanana na sokwe. Aidha, walitembea kwa kupinda mgongo kama kibiongo. Chakula na uhai wao ulitegemea kukusanya matunda, kokwe, majani ya miti na mayai ya ndege. Vile vile, walitegemea wanyama wadogo, kufukua mizizi na kubambua magamba ya miti walipoka na njaa.

Maisha yao yalikuwa ya hatari. Walikuwa wakiwindwa wanyama wakubwa. Hii ni kwa sababu mwanzoni hawakuwa na silaha za kujihami. Hivyo iliwabidi kujificha katika miti na vilima kuepuka uvamizi. Lakini usalama wao ulitegemea kwa kiasi kikubwa kudura za Mungu au pengine miungu.

Kwa taratibu wanadamu hawa walijifunza kutengeneza silaha. Walianza kwa kutumia fimbo nene zenye ncha au mawe ya kutupia. Baadaye walichonga mawe ili kuyafanya kuwa visu, nyundo au vigumba vya mikuki. Hatimaye, walivigomoa au kupasua vipande vya mawe na kuvitumia kama mishale. Hapa ndipo walipoanza kuwinda wanyama wakubwa, mithili ya swara, nguruwe, nyati na ngiri. Pia waliweza kutumia mikuki kudunga samaki majini.

Mababu zetu hawakuwa na nymba. Kwanza walikuwa wakijisitiri kwa kukaa chini ya vivuli vya miti au kujenga vibanda vya matawi na majani ya miti. Hawakuweza kuingia mapangoni asilani kwa kuchelea wanyamapori wakali kama Chatu, Simba, na Mamba waliokaa humo. Kwa bahati, siku moja mmoja wao aligundua moto alipokuwa akipekecha vijiti. Kabla ya ugunduzi huu, wao pia wahakujua kazi ya moto na walikuwa wakiogopa na kukimbia moto jinsi wafanyavyo wanyama wa mbugani mpaka leo.

Ujuzi wao wa kutumia moto ulileta mabadiliko makubwa. Baada ya hapo waliweza kukaa mapangoni na kukoka mioto milangoni mwa mapango ili kuwaogofya adui. Halikadhalika, waliweza kuota moto, kumulikia maskani yao mapya na kuchoma nyama badala ya kuila mbichi.

Wanadamu wa awali hawakuwa na mavazi. Waliwezaje kuzuia barid? Inadhaniwa kwamba nywele nyingi walizokuwa nazo kwenye mwili zilisaidia kuwapa joto. Uvaaji wa nguo ulianza walipoanza kutumia ngozi kutoka kwa wanyama waliowawinda. Walizisafish ngozi kwa kuzipaa kwa kombe za mawe na kuzianika juani. Zilipokuaka walizivaa kwa kujifunga na kuzishikanisha kwa mifupa au mikanda ya ngozi.

Wanadamu hawa hawakuweza hata kuongea. Waliwasilian kwa kupiga mayowe, kutoa milio au kunguruma jinsi wafanyavyo wanyama. Polepole walianza kutumia sauti na baada ya muda walizipanga sauti kuibua mfumo wa maneno yenye maana za kipekee. Umilisi wa kutumia lugha uliwawezesha kupiga hatua kubwa kimaendeleo. Lugha pamoja na matumizi ya moto na silaha viliwarahisishia maisha na kuwawezesha kupata muda wa kupumzika mapangoni jioni wakiota moto. Kutokana na hali hii waliweza kutekeleza jambo moja kuu waliloturithisha. Walitupokeza sanaa. Kutoka kwao tulirithi fasihi simulizi na kupata nakshi za michoro yao kwenye mapango. Michoro hii inapatikana katika mapango hata leo hii nchini Ufaransa, Uhispania, Afrika Kusini na hata Afrika Mashariki.

- a) Fupisha makala uliyosoma kwa maneno yasiyopungua 120 wala kuzidi 150.
(alama 12, utiriko 3)

Maandalizi

Nakala safi

3. Matumizi ya Lugha (Alama 40)
- a) Andika sentensi zifuatazo kwa kutumia kirejeleo cha ngeli kifaacho (alama 3)
- i) Sungura alishinda kobe katika mbio hizo
 - ii) Chura alisafisha vyoo vizuri
 - ii) John amekata nyasi yote

b) Ainisha viambishi katika maneno uliyopewa

i) Mshindi

(alama 1)

ii) Mkate

(alama 1)

iii) Kujidhiki

(alama 1)

c)i) Mofimu ni nini?

(Alama 1)

iii) Taja aina mbili za mofimu na kwa kila aina utolee mifano miwili (alama 3)

d) Eleza sifa bainifu za sauti zifuatazo

i) (p) na (b)

(alama 2)

ii) (i) na /u/

(alama 2)

e) Tunga sentensi kuaonyesha matumizi manne ya kiimbo.

(alama 4)

f) Onyesha matumizi manne ya silabi zifuatazo.

i) ku

(alama 2)

ii) ni

(alama 2)

g) Tunga sentensi ukitumia vitenzi ulivyopewa katika kauli ya kutendewa

i) la

(alama 1)

ii) lea

(alama 1)

iii) ficha

(alama 1)

h) Eleza matumizi manne ya kistari kifupi.

(alama 1)

i) Sahihisha sentensi zifuatazo

a) Msichana ambaye anayelia anaitwaje?

b) Katika sarufi ya Kiswahili kuna njia tofauti za kuonyesha mazoea. Kwa kutunga sentensi onyesha njia tatu zinazonyesha hali ya mazoea.

(alama 3)

- j) i) Tunga sentensi moja kuonyesha tofauti ya maneno matatu yafuatayo. **Teka, tega, tenga.** (alama 3)

- ii) Andika maana mbili tofauti za maneno ya fuatayo.
Mbiu (alama 1)

Kina (alama 1)

- k) Andika kwa ukubwa na udogo sentensi ifuaayo:
Mbwa wa mzee ameuawa na ndovu mweusi
ukubwa (alama 1)

udogo (alama 1)

- l) Bainisha nomino katika sentensi ifuatayo na ueleze ni za ina gani. (alama 3)
Askari jela alishikwa na wasiwasi alipokabiliwa na halaiki ya wafungwa.

- m) Andika sentensi zifuaazo kulingana na maagizo. (alama 4)
i) Nikimuona baba nitamueleza yote (kana)

ii) Asiye na mtoto aelekee jiwe (sahihisha)

- iii) Sisi ndisi tufiowaokoa (Andika umoja)

iv) Njeri atakuja shuleni. Njeru atachelewa (unganisha iwe sentensi moja)

n) i) Mahali palipohama huitwa _____ (alama 1)

ii) Sehemu ya mkono wa binadamu inayovaliwa saa huitwa _____
(alama 1)

Isimu Jamii – alama 10

Ni kawaida katika mazungumzo watu kufanya makosa ya kisarufi, uteuzi au matumizi ya msamiati na mantiki. Kwa kutoa mifano maridhawa jadili sababu (tano) tofauti tofauti zinazosababisha makosa haya. (alama 10)

Fasihi – alama 20 Mstahiki Meya, T. Arege.

Fafanua shida kumi (10) zilizowakumba wanacheneo chini ya uongozi wa Meya Sosi.